**Yesmark Tuition Services**

**YESMARK TUITION SERVICES**
**IDARA YA KISWAHILI**
**KISWAHILI**
**DES 2015**
**MUDA: SAA 2½**

**KARATASI 102/2: UFAHAMU, UFUPISHO, LUGHA, ISIMU JAMII**

**SEHEMU A: UFAHAMU - ALAMA 15**

Alibarikiwa kwa viungo vyote vya mwili, vizito na vyepesi, vikubwa na vidogo, ila kimoja kionekanacho kidogo kuliko vingine ndicho kilichokuwa mfalme wa vyote vingine. Nacho hiki *kilimchongea* kweli. Wasemao husema, 'mti huchongekwa na tundaze'. Naye huyu tuliyempagaza jina 'Chokochoko' alichongewa pakubwa na ulimi wake uliozitambua tu ndimi za moto ulizolamba au kutapika kiholela. Na tutupe jicho tuone vituko vya ulimi huu.

Si umbeya huo! Alikuwa *kilimilimi* hivi kwamba chochote alichonasa kutoka kwa yeyote awaye yule, sharti angekiwasilisha na <u>*kumtaarifu*</u> mwingine. Hakujali lilisemwa na nani au kwa nini. Hata mambo ya faragha ya baraza la wazee angeliingilia tu, sijui akiwa mgeni wa nani, kisha angelisambaza hata kwa *chokora* na vigoli. <u>*Udukizi*</u> wa namna hii ulimpelekea kuwa na *rabsha* baina yake na wote waliomzunguka. Kila aliyemwona akikaribia alijaribu kuyafunika maneno yake hadi apite'. Msemo 'funika kombe mwanaharamu apite' ukawa wamlenga yeye.

Waaidha ulimi wake ulikuwa *ulimi wa upanga*. Kungalikuwa na mashindano ya kukaripiana, neno la kwanza la Chokochoko ndilo lingalimpiga dafrao mpinzani wake hata ajiuzulu mara moja. Alifikiri maisha ni jukwaa la mashindano na kwake yeyote aliyekuwa na *upyaro* wa msimu ndiye angeshinda. Maneno yake yote yalikuwa mfano wa sumu ya joka kali. Naye kwake, hili lilikuwa na hasara pia – aliuvaa uso usiofurahi, kila wakati umekunja peto, midomo imekunjana na uso umejaa <u>*makunyanzi*</u> kama wa mzee wa miaka mia moja. Mgeni yeyote aliyemwona na kusikia kuwa alikuwa mtoto ambaye hata ubwabwa haujamtoka shingoni alimaka.

Chokochoko pia alikuwa mcheza shere. Ukweli ukawa neno lisilo na maana kwake. Hakuiona ahadi kuwa deni. Kazini angeahidi jambo fulani wala hangelitimiza abadani. Mkutanapo angekupiga chenga kukudanganya. Angekupaka mafuta kwa mgongo wa chupa na uridhikapo na kwenda, angeahirisha utekelezaji wa ahadi yenu hadi mtakapokutana tena. Kwa mtendewa, hii ilikuwa dhihaka iliyokithiri. Yamkini mtu kama huyu huweka nadhiri hata kwa Mungu asiitimize, nayo thawabu ataipataje?

Uchokochoko wake ulimfanya awe ndumilakuwili. Ukichunguza ulimi wake, jamaa huyu alikuwa *kisebusebu*. Akimuona yeyote akinawiri angejitokeza kama *aliyeteremea* mno na mwenye kusherehekea pamoja na apataye. Hili lingefanya



www.yesmarkeducation.com

aliyelengwa kumfunulia moyo wake wote na kuuacha wazi kwake amchunguze atakavyo. Maadui wangevutwa kwa ulimi. Kuna alioibiwa, kutapeliwa, kuhujumiwa kwa mioto au kwa namna zozote zile; wengine waliuliwa kutokana na hila zake. Kumbe atafuta jinsi ya kufaidika yeye!

Naye avumaye baharini papa kumbe wengine wapo! Ukiua kwa upanga, kwa upanga pia utakufa. *Chokochoko* za Chokochoko zikawabughudhi vijana wengi kwa muda mrefu nao wakampangia njama, wakatumia njia ile aliyoitumia kulipizia kisasi – ulimi mtamu. Walijua kuwa yeye alipenda kuutumia ulimi wake kupata sifa. Wakati huo makachero walikuwa wakichunguza kwa bidii vianzo vya visa mbalimbali vya uhalifu kijijini humo. Wakajua kumsifu kwa kiasi kidogo tu kungemfanya kujisahau na kuelezea siri zake zote.

Licha ya kuutumia kuropoka, ulimi wa Chokochoko pia ulitumiwa *kuchapa maji*. Siku ya mtego, vijana hao walijifanya wakarimu kweli kweli, wakamununulia kileo. Alipokwisha uchapa *ugimbi*, vijana wakaanza kumsifu Chokochoko kwa ujanja huku wakiwakashifu watu mbalimbali waliojua walikwisha hasiriwa na *afriti* huyu. Kusikia sifa zake zainuka, alianza kutokwa na maneno bila mpango, huku akieleza namna alivyowashusha wote hao kwa jinsi mbali mbali – kuna aliowapangia kuuawa, kuibiwa, kuchomewa nyumba na kadhalika.

Wakati wote huu, kachero mmoja alikwisha karibia akiwa na kiredio cha kunasia sauti. Akisha boboka bobobo, makachero wawili wakajitokeza, wakajitambulisha na kumfahamisha Chokochoko shughuli zao pale. Alipojaribu kujitetea kiredio kikafunguliwa, akayasikia yote aliyosimulia. Akalevuka pale pale, akawaangalia wale vijana majirani ambao sasa walikuwa wakitabasamu. "Twende kituoni!" Makachero wakamwamuru. Waliokuwapo wakajisemea nyoyoni, "Kweli heri kwaa ya dole kuliko ya ulimi."

**Maswali**

(a) Andika anwani mwafaka ya ufahamu huu. (alama 2)

(b) Taja tabia tatu kuu za Chokochoko. (alama 3)

(c) Eleza dhana ya ndumilakuwili kulingana na mwandishi. (alama 2)

(d) Eleza maana ya "Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo! Kama ulivyotumiwa kwenye kifungu. (alama 3)

(e) "Alikuwa mtoto ambaye ubabwa haujamtoka shingoni" ina maana gani? (alama 2)

(f) Maneno haya yana maana gani kulingana na kifungu. (alama 3)
   i) Udukizi Kumtaarifu
   ii) Makunyanzi

## SEHEMU B: UFUPISHO - ALAMA 15

Kwa kawaida, binadamu huishi kwa kutangamana na binadamu wenzake. Katika kutangamana huku, watu huathiriwa kitabia, kifikira, kimavazi na kimaisha kwa jumla. Watu wote katika jamii wana uwezo wa kuathiri na kuathiriwa na wenzao wa umri mmoja. Hata hivyo, walio katika hatari ya kuathiriwa zaidi na mahirimu wao ni vijana. Hali hii ya kuathiriana huitwa shinikizo-rika au shinikizo-marika. Vijana huaminiana na kuthaminiana sana. Kwa sababu hiyo, ni rahisi sana kuingizwa katika mitego na wenzao. Isiaminiwe kuwa vijana pekee ndio wanaoathiriwa na shinikizo-rika. La hasha! Watu

www.yesmarkeducation.com

wazima pia huwafuata wenzao mithili ya bendera kufuata upepo. Mwenzake akinunua gaqri, yeye pia hukimbilia mkopo kununua gari la sampuli iyo hiyo bila kuwaqzia kima cha kibindo chake.

Wataalamu wa saikolojia kuwa kukabiliana na tatizo la shinikizorika si rahisi kwa sababu shinikizo-rika huleta mtafaruku wa kinafsi akilini mwa anayeathiriwa. Nafsi moja humshawishi kufuata wenzake huku nyingine ikimnasihi kuandama upekee au ubinafsi wake. Shinikizo- rika huathiri sana mahitaji ya kimsingi ya binadamu. Ikumbukwe kuwa mahitaji haya ya kimsingi ni ya kila mwanadamu, nayo ni kama vile kupata lishe, hewa safi, kupenda na kupendwa miongoni mwa mengine. Kila mtu hutaka kujihusisha na kundi la watu ambao watamfanya kuhisi kuthaminiwa na kukubalika. Kutokana na haja ya kutaka kukubalika, anayetaka kutambuliwa huridhia matakwa ya wenzake bila hata kuyawazia.

Shinikizo-rika hujitokeza kwa sura nyingi. Mathalani, vijana huwafanya wenzao kuona kuwa wana hatia wasipoafiki kutekeleza kama wanvyoshinikizwa. Kauli kama vile 'tulifikiri wewe ni mmoja wetu' au 'usiposhirikiana nasi utakuwa umetuvunja moyo' hutamalaki. Wanaokataa hubezwa na kufanyiwa stihizai na wenzao na hata kutengwa. Vitisho hutolewa, wakati mwingine, an anayeshinikizwa akidinda, mabavu hutumika.

Ni muhimu kwa watu, hasa vijana, kufahamu kuwa shinikizo-raka lipo na wanapokabiliwa na tatizo hilo, watambue kuwa wana haki ya kusimama kidete kutetea msimamo wao dhidi ya wenzao. Kumbuka, baridi huwazizima kondoo kwa namna tofauti.

Kama njia moja ya kukabiliana na shinikizo-raki, wanasaikolojia wanapendekeza watu kujiamini na kuelewa kwamba wana haki ya kuwa tofauti na kuwa na upekee wao. Mtu anapojiamini na kushikilia msimamo wake, anaweza kujiepusha na madhara yatokanayo na shinikizo-rika. Asiyejiamini huwa mwepesi sana wa kuingizwa katika lindi la mashaka na wenzake.

1. Bila kupoteza maana, fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno 40.
   (alama 8, 1 ya mtiririko)
2. Fupisha mambo muhimu ambayo mwandishi amezingatia katika aya tatu za mwisho. (maneno 30) (alama 7, 1 ya mtiririko)

www.jesmarkeducation.com

## SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA - ALAMA 40

a) Yakinisha katika **wingi**.
   Hakutuarifu kuhusu yule hajala. (Alama 1)
b) Fafanua Kwa kutungia sentensi **matumizi** mawili ya neno **namna**. (alama 2)
c) **Pambanua** sentensi ifuatayo kwa kutumia kielelezo cha **jedwali**. (alama 4)
   Kalamu mpya ni ya mwalimu.
d) Vinyambue vitenzi vifuatavyo kulingana na maagizo. (alama 2)

a. Ja ________________________________ (tendwa)
b. La ________________________________ (tendesha)
c. Nata ______________________________ (tendeshwa)
d. Juvya _____________________________ (tenda)

e) Tunga sentensi **moja** ili kudhirisha matumizi ya viwakifishi hivi:
Mdokezo, mshazari. (alama 2)

f) Eleza maana ya **mofimu**. (alama 1)

Bainisha aina za **mofimu** katika maneno yafuatayo.

i) Lakini
ii) Kiti (alama 2)

g) Eleza maana **mbili** katika sentensi hii. (alama 2)
Majambazi walimwibia Letangule gari jipya.

h) ***Tambua na ueleze aina za Shamirisho katika sentensi ifuatayo***. (ala 2)
Yusufu alimnunulia simu mpenzi wake.

i) ***Onyesha virai vitatu katika sentensi hii na utaje ni vya aina gani.*** (ala.3
Yule mdogo amekunywa maziwa kwa kikombe.

j) ***Andika kinyume cha***: (ala.1)
Walizama walipokuwa wakikusanya mchanga.

k) ***Geuza sentensi hizi ziwe katika usemi halisi*** ( ala. 4)

i. Mwenye hoteli alitaka kujua jumla ya vikombe vya chai tulivyohitaji.
ii. Mtoto alisema kuwa angewatembelea kwao mwezi amabo ungefuata.

l) ***Andika sentensi ifuatayo katika wingi hali ya udogo*** ( ala.2)
Kitabu kilichonunuliwa hakimfai mwanafunzi huyu

m) ***Hii ni nomino ya aina gani?*** (ala.1)
Wema

n) Tofautisha vitate hivi. (alama1)
Kipofu/kibofu

o) Ainisha sentensi ifuatayo: (Alama 2)
Mwalimu mgeni atakaa kwake.

p) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya kiambishi. (Alama 2)

i) 'ka'
ii) 'Ji'

q) Geuza sentensi hii hadi udogo: (Alama 1)
Nyoka yule mrefu alifukuzwa na watu wengi.

r) Tambua na ueleze vitenzi vilivyotumika katika sentensi ifuatayo. (Alama 4)
Shipiri ni mzuri ingawa huenda akaharibiwa na Halima ambaye si msichana mwema.

s) Tambua mzizi katika neno: (alama 1)
Msahaulifu

## SEHEMU D: ISIMU JAMII - ALAMA 10

www.yesmarkeducation.com

a) Kuna nadharia tatu zinazohusu asili ya lugha ya Kiswahili. Zijadili huku ukionyesha kufaa au kutofaa kwake. (alama 6)

b) Eleza sifa za lugha ya taifa (alama 4)

www.yesmarkeducation.com